MAONESHO YA 41 YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM

VIGEZO VINAVYOTUMIKA KATIKA KUSHINDANISHA MABANDA BORA

1.0 Uchaguzi wa Mabanda bora

Washiriki ambao watapenda kushindanishwa kwenye zoezi la kutafuta Banda bora waekezwa kujisajili TanTrade kabla ya Maonesho hayajaanza. Washiriki watachagua kundi moja tu ambalo watataka kushindanishwa.

VIGEZO VYA KUCHAGULIWA

i. Muonekano wa jumla wa Banda la Maonesho

Majaji watatazama muonekano wa ujumla wa Banda la Maonesho kwa kutoa kipaumbele kwamuonekano bora unaowavutia wateja. Vipengele muhimu vinavyotazamwa ni pamoja na:

- Muonekano wa Kitaalamu (Jinsi gani banda linavutia macho ya mtazamaji /mtembeleaji)
- Upangiliaji wa rangi (katika banda) na usafi
- Alama zinazoonekana na michoro ya grafu kwa ajili ya kutoa maelezo
- Vitu au kifaa kinachozunguka zunguka au kutembea kuvutia macho ya watembeleaji
- Usafi wa Banda

ii. Muonekano wa kitaalamu wa Bidhaa au Huduma

Jaji atapima uwezo wa banda kwa jinsi linavyoonesha bidhaa au huduma kwa watembeleaji kwa ufanisi. Vipengele vifuatavyo vitatazamwa:

- Mpangilio wa bidhaa/ huduma zinazofanana ili kuzifanya zionekane vizuri
- Mpangilio wa bidhaa kwa mtiririko unaofaa

- Matumizi bora mabango, picha, ufundi, vifaa, rangi za pamoja
- Matumizi sahihi ya taa (spot lights) kwaajili ya kuelta mwanga Bandani
- Mpangilio mzuri unaowezesha mteja kuona bidhaa kwa urahisi (Bidhaa isiyorundikana bilaa utaratibu)
- Ubunifu unaotumika katika kuonesha bidhaa au huduma kwa walengwa/watembeleaji

iii. **KiwangonaUborawaBidhaaauHuduma**

Tathminiyauboraitaangaliwailikutofautishabidhaaau hudumakatiyaBidhaa/Hudumazilizobora au duni. Vipengelevifuatavyovitawasaidiamajajikutathminiubora:

- Ujuzi / sifazakitaalamu, uzoefu
- Usanifuwahudumanabidhaa
- Utendaji, matumiziyabidhaa au huduma
- Utayariwakutumika/umaliziaji/ ufungashajinamaandishikwenyekifungashio
- Taarifakuhusuuwezowauzalishajikwakipindikisichopunguamiakamitatu (3) nyuma
- Usajiliwa TBS / ISO, Bar code, TFDA pale inapohusika

iv. UhusianonaKauliMbiuyaMaonesho

Majajiwatatathminiufanisiwabandakatikakuonyeshabidhaa au hudumanaiwapoMuonyeshaji/ MshirikianafahamuchochotekuhusuKauliMbiunaamepangiliabidhaayakeiliushiriki wake uwenaufanisi

KAULI MBIU: UKUZAJI WA BIASHARA KWA MAENDELEO YA VIWANDA

v. Taarifakuhusubiasharanausimamiziwabanda la Maonesho

Waonyeshajikatikabandawanatarajiwakuwanaujuzikuhusubidhaaau hudumawanazoonesha.
Majajiwanawezakuulizamaswalimachacheyakitaalamuilikupatataarifayabiashara, zanazakujitangaza, kadizamawasiliano, vipeperushin.kambavyowatembeleaji au watejawanawezakupewa.
Washirikimakiniwanatarajiwakuwanataarifazotemuhimukwaajiliyakufanikishalengo la kushirikikatikaMaonesho. Mambo yafuatayoyatachunguzwazaidi:

- Mfanyakazi mwenye ujuzi na makini mwenye uwezo wa kujibu maswali vizuri na kwa ufupi
- Upatikanaji wa vipeperushi (katalogi ya bidhaa) na nyaraka nyingine za kupokelea oda (maulizo) yatakayopatikana
- Kadi za mawasiliano
- Bango/ Ubao wa kuonesho jina la kampuni, kitabu cha wageni na mawasiliano ya kiofisi

vi. Huduma kwa Wateja

Majaji wataangalia muonekano wawafanyakazi wa Banda, huduma zitolewazo, Umakini wa Wafanyakazi kwenye Banda na hata wanavyotoa huduma katika hali ya kawaida kwenye biashara yao nje ya Maonesho.Mambo yafuatayo yatawasaidia Majaji kupima ubora wa huduma kwa wateja**;**

- Salamu (mchangamfu, asiye na majivuno na anayesikika)
- Muonekano wa utanashati
- Lugha ya mwili (jinsi ya ukaaji, wasiwasi, aibu, kukunja mikono nk)
- Kuwa makini na kutumia mawasiliano ya macho (kutazamana ana kwa ana)
- Uwezo wa kujibu maswali kwa ufasaha, kutoa maelezo ya wateja kwaajili ya ufuatiliaji baada ya Maonesho
- Jinsi ndani ya muda mfupi Mfanyakazi anaweza kujieleza na kuitambulisha kampuni/ bidhaa zinazoonyeshwa
- Jinsi ya kumpokea mteja anapoingia Bandani

2.0 TUZO KWA MAKUNDI MAALUM

Kwa kuwa Lengo Kuu la Maonesho ni kukuza biashara za ndani na nje ya nchi, makundi mawili maalum ya waoneshaji hupewa tuzo maalum ili kutambua mchango wao katika soko la ndani na nje ya nchi. Makundi hayo ni "Mshiriki Anayeonesha Bidhaa Bora Anazouza Nje ya Nchi na Mshiriki Anayeonesha Bidhaa Bora Kwaajili ya soko la ndani". Washiriki watakaopenda kushiriki katika makundi haya wanatakiwa kujisajili TanTrade kabla yaMaonesho hayajaanza. Kundi jingine muhimu ni Mshindi Bora wa Maonesho

2.1Vigezo kwa mshiriki bora wa Bidhaa Zinazouzwa Nje ya Nchi.

Jopo la majaji wataangalia na kupima vipengelevifuatavyo katika kutathmini na kumpata mshiriki bora wabidhaa za Tanzania zinazouzwa nje ya nchi;

- Uongezaji wa thamani kwa bidhaa inayoonyeshwa
- Uthibitisho wa ubora kutoka vyombo vya udhibiti vya ndani au vya kimataifa pale inapobidi
- Ufungashaji (ufungashaji wa mwanzo na ufungaji wa pili) na uwekaji wa chapa katika bidhaa)
- Ustadi na Ubunifu katika kuonyesha bidhaa/huduma
- Uwezo wa uzalishaji na takwimu za uuzaji wa nje (kwa miaka mitatu (3) mfululizo)
- Uonyeshaji wa bidhaa- jinsi bidhaa inavyoonekana/inavyofanya kazi/ inavyotengenezwa.
- Masoko ya nje ambako Kampuni inauza bidhaa yake, Ushiriki katika Maonesho ya Biashara za Kimataifa (nchi zipi alizoshiriki)
- Ustadi au utaalamu katika kutoa huduma
- Vitu dhahiri au vifaa vinavyotumika katika kutoa huduma
- Mawasiliano – utoaji wa taarifa kwa wateja katika lugha watakayoweza kuelewa
- Kutumainiwa-Utendaji usioyumba bali wa kumhakikishia mteja kupata huduma hata baada ya mauzo

2.2 Vigezo kwa mshiriki bora wa Bidhaa za Ndani

Jopo la majaji litaangalia na kuzingatia vipengelevifuatavyo katika kutathmini na kumpata mshiriki bora wabidhaa za ndani;

- Ongezeko la thamani kwa bidhaa
- Uthibitisho wa ubora kutoka Taasisi za ndani kama vile:TBS, TFDA
- Ufungashaji (Fungashio la ndani na la juu) na uwekaji wa chapa katika bidhaa
- Ubunifu na uvumbuzi
- Uwezo wa uzalishaji na kiasi cha mauzo (kwa miaka mitatu (3) mfululizo)
- Uwasilishaji wa bidhaa - jinsi bidhaa inavyoonekana
- Mtandao wa usambazaji bidhaa katika soko la ndani (hasa katika maeneo ya vijijini)
- Ustadi au utaalamu katika kutoa huduma
- Mawasiliano – utoaji wa taarifa kwa wateja katika lugha inayoeleweka
- Kutumainiwa-Utendaji usioyumba bali wa kumhakikishia mteja kupata huduma hata baada ya mauzo
- Ushiriki katika Maonyesho ya ndani kama DITF, SIDO, Nane Nane n.k
- **ZINGATIA**: Majaji lazima waridhike kwamba thamanikubwa imeongezwa kutoka malighafi ya ndani (Tanzania)

2.3 Mshindi wa Jumla wa washiriki wote.

Mshindi wa Jumla atapatikana katika duru ya pili ya ushindanishaji utakaofanywa na Jopo la Majaji ambaowatamchagua mshindi wa Kwanza kutoka kila Kundi kwakutumia vigezo vilivyotumika katika kuamua washindiwa mwisho katika makundi ya kawaida

Hata hivyo, Majaji watatumia vigezo vyote kwa ujumla katika kupima banda. Majaji hawatajitambulisha